MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

Cheche za Fikra

JUZUU 4 TOLEO 12

NOVEMBA 4, 2008

KIJARIDA CHA BURE— UKISHASOMA MPE MWINGINE—USIBANIE!

SIKU YA HISTORIA NOV 4, 2008

RAIS MTEULE BARACK OBAMA!



Rais Mteule wa Marekani Barack Obama

Na. Fred Katunzi

Seneta Baraka Hussein Obama wa Jimbo la Illinois nchini Mmarekani amechaguliwa kwa kishindo kisicho na utata wala makeke kushika nafasi ya kiti cha Urais wa Marekani katika uchaguzi mkuu Rais, Wawakilishi, Maseneta na nafasi mbalimbali uliofanyika jana Jumanne nchini humo.

Ni ushindi wa kihistoria

Seneta Obama kutoka chama cha Demokrati ameshinda baada ya kumbwaga vibaya mpinzani wake kutoka chama cha Republikani Seneta John Sidney McCain wa Jimbo la Arizona.

Kwa ushindi wake huo Seneta Obama anakuwa Mmarekani wa kwanza mwenye asili ya Afrika kushika wadhifa wa juu kabisa katika serikali ya nchi hiyo tangu Taifa hilo lilipoundwa kufuatia vita vya mapinduzi mwaka 1776 vilivyotenganisha makoloni ya Uingereza katika bara la Marekani.

Seneta Obama mwanasiasa ambaye jina lake lilikuwa halijulikani sana miaka miwili iliyopita aliibuka kama kipenzi cha wapiga kura wa chama cha Demokrati pale alipotoa hotuba ya kusisimua sana kwenye Mkutano Mkuu wa kuchagua mgombea wa chama hicho mwaka 2004 na kuwa gumzo la watu wengi kuanzia siku hiyo.

Wakati huo Seneta Obama ndiyo tu alikuwa ameanza kunuia kuingia katika siasa za kitaifa pale alipoamua kugombea kiti cha Useneta wa Jimbo la Illinois (kila Jimbo linatoa Maseneta 2, na kuna majimbo 50) ambapo jiji lake maarufu ni lile la Chicago.



Ushindi wake wa kupata kiti cha Seneta ilikuwa ni kama alama ya nyota yake ya kisiasa kung'ara zaidi na kuanzia wakati huo jina lake lilianza kutajwa katika nafasi ya Urais pale Rais anayemaliza muda wake Bw. George Bush wa Repablikani atakapomaliza muda wake.

Hata hivyo safari yake ya kueleka Jumba Jeupe (Ikulu ya Marekani) haikuwa rahisi kwani ilikutana na kila aina ya vikwazo vya

(inaendelea Uk2)



Benjamin. G. Mwalukasa

Kijarida Ulichoshika

- **Kinatoka kila Jumanne**
- **Ni cha bure kabisa!**
- **Kisichofungamana na chama chochote au fisadi yeyote!**
- **Kiko huru, kinathubutu, na hakiogopi mtu au hoja yoyote.**
- **Ni kijarida chako!**
- **Haki zote za kuchapa na kunakili zimeruhusiwa!**

HOJA YA MWANAKIJIJI — ZIMERUDI TOKA WAPI?

Mazingaombwe ni fani ya kumfanya mtu aamini kuwa mfuko ambao ulikuwa mtupu mara moja umeweza kutoa njiwa bila kuweza kuona njiwa hao walitoka wapi.

Niliposikia kwa mara nyingine tena kuwa zaidi ya shilingi bilioni 69 zimerudishwa kufuatia majadiliano ya serikali na waliolipwa fedha za EPA kinyume cha sheria mwanzoni nilitaka kufurahi.

Lakini nikiwa nafahamu vizuri fani ya mazingaombwe nikaanza kujiuliza kama hizi fedha zilikuwa hazipo, waliochukua wameenda kuzitumia, sasa hawa waliozirudisha walirudisha fedha hizo kutoka wapi?

Niliposikia kuwa kuna wengine wamezirudisha fedha taslimu katika mifuko nimezidi kuchanganyikiwa kuwa hizi fedha zote ni halali kweli? Kama ndiyo kwa muda wote huu walikuwa wameziweka wapi?

Sitarajii majibu ya maswali hayo.

Ndani ya Toleo Hili

Ushindi wa Obama	1, 2
Zimerudi toka wapi?	1
Wazee walipoizidi TISS	2
Wazee walipoizidi TISS	3
Zilizorudishwa ni 52%	3
Maoni ya Mtandao	4
Picha na Katuni	4

HABARI MBALIMBALI

WAZEE WAWAZIDI USALAMA WA TAIFA

Na. Mahmoud Rashid



Wale wazee wanaodai kuwa hawajalipwa mafao yao kutoka iliyokuwa jumuiya ya Afrika ya Mashariki hatimaye walifanikiwa kuvizidi ujanja vyombo vyote vya usalama nchini na kusababisha adha kubwa kwa watumishi, wananchi na wafanyakazi mbalimbali.

Wazee hao ambao mara kadhaa wamejaribu kukusanyika kwenye viwanja wa Ikulu na kujaribu kuandamana siku za hizi karibuni wameonesha kuthubutu zaidi katika kudai kile ambacho wanaamini kuwa ni haki yao.

Mapema siku ya Jumatano wazee hawa wakiwa wameweza kujipanga vizuri na kufika eneo walilokubaliana bila kugundulika waliweza kuingia barabarani eneo la makutano ya Barabara za Ally Hassan Mwinyi (zamani Bagamoyo) na Umoja wa Mataifa na kukaa katikati ya barabara.

Idara ya TISS ilishindwa kugundua mpango huu!

Kitendo hicho ambacho kinaonesha wazi kuwa hakikutarajiwa na vyombo vyetu vya usalama kilisababisha msongamano mkubwa wa magari ambayo yalishindwa kuingia katikati ya jiji kwa shughuli mbalimbali.

Uchaguzi wa barababara hiyo badala ya



barabara nyingine kama ile ya Morogoro au ya Kilwa inaonesha ni jinsi gani kundi la wazee hawa waliweza kufanya maamuzi ya kimkakati wakitarajia athari zaidi.

Barabara hiyo hutumiwa na viongozi wengi wa nchi, mkoa na pia mabalozi mbalimbali na wawakilishi wa Jumuiya

RAIS MTEULE OBAMA (KUTOKA 1)

vya kila aina Kisiki cha kwanza ambacho Seneta Obama alikumbana nacho na kukishinda ni kura za maoni zilizomkutanisha yeye na wagombea wengine wa Demokrati akiwemo mpinzani wake mkubwa ndani ya chama Senera Hillary Clinton (Mke wa aliyekuwa Rais wa nchi hiyo Bill Clinton).

Kinyang'anyiro cha ushindani huo kilidumu kwa miezi kadhaa lakini hatimaye chama chake kilimpendekeza kuwa mgombea wa Urais katika mkutano wake wa mwezi wa nane huko Colorado.

Hata hivyo kimbunga cha Obama nusura kiparaganyike pale video ya kiongozi wake wa kiroho Mch. Wright ilipoibuka na kumuonesha mchungaji huyo akihubiri kwa jazba kubwa na kutumia maneno ya kuilaani Marekani na kutoa tuhuma nzito dhidi ya watu weupe.

Kwa umahiri mkubwa na mkakati mzito Seneta Obama aliweza kukwepa mtego huo uliomhusisha yeye na kiongozi wa kiroho pale alipoamua kutoa hotuba ambayo inaaminiwa na watu wengi kuwa ilichambua tatizo la rangi za watu kwa kina. Seneta Obama ambaye mama yake ni mzungu na baba yake kutoka Kenya alifanikiwa kuwashawishi wananchi wa Marekani kuwa haamini mambo anayoamini mchungaji Wright.

Wachunguzi wa mambo ya kisasa wanaelezea ushindi wa Obama kuwa umetokana hasa na watu kuchoshwa na mwelekeo wa kisiasa wa Taifa hilo kubwa na zaidi sana hali ya kiuchumi ambayo imeathiri mataifa mengi duniani. Zaidi ya yote, ushindi huo umekuja baada ya watu kuona utawala wa chama cha Repablikani chini Rais Bush ukitetereka katika masuala mengi na hivyo wangependa kuanza upya.

Wachunguzi wengine wanaamini kuwa Seneta Obama amepata ushindi huo hasa kwa sababu ya ahadi yake ya kuviondoa vikosi vya Kimarekani kutoka Iraq na kuanza mazungumzo ya kuleta amani na nchi mbalimbali duniani hasa Iran.

Pamoja na hayo wachambuzi wa mambo ya kisiasa wanaamini kuwa kitu kingine kilichomsaidia Seneta Obama ni mpangilio wa kampeni yake jinsi ambavyo ulitumia mbinu zilizotumiwa na Rais Bush mwaka 2004 pale alipotuma mamia ya watu kutembea nyumba kwa nyumba kushawishi watu wampigie kura.

Hilo liliwezekana ukizingatia uwezo mkubwa wa fedha ambazo Seneta Obama aliweza kuchangisha kutoka kwa watu mbalimbali na taasisi.

Ahadi kuu ya kampeni yake ilikuwa "Mabadiliko yanakuja" na mashabiki wake walisikika wakiimba na kurudia maneno ya "Ndiyo, Tunaweza".

Kwa hakika wameweza.

Katika salamu zake za kukubali kushindwa Seneta John McCain alimtakia mafanikio mema na afya njema Seneta Obama na kuwashukuru wananchi wa Marekani kwa kumpa nafasi ya kugombea Urais.

Katika hotuba yake Seneta Obama aliwahakikishia Wamarekani mabadiliko wakiwa pamoja naye na kwa watu wa nje ya Marekani aliahidi "pambazuko jipya la uongozi wa Marekani".

Seneta Obama alizaliwa tarehe 4 Augusti, 1961. Rais mteule Obama anatarajiwa kuapishwa tarehe 20 Januari, 2009 kushika kiti cha Urais wa Marekani kwa kipindi cha miaka minne ijayo. Atakapoapishwa atakuwa ni Rais wa 44 wa Marekani.

Makamu Rais Mteule ni Seneta Joe Biden wa Jimbo la Delaware.

Bw. Obama ana mke Michelle Obama na watoto wawili Sasha na Maria.

MPATIE MTU MWINGINE BURE

WAZEE WALIPOIZIDI TISS

mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa. Jinsi wazee hawa walivyofanikiwa inaonesha ni jinsi gani Taasisi muhimu ya Usalama

wa Taifa ambayo inaongozwa na Bw. Rashid Othman imeendeleza rekodi yake ya kushindwa kuzuia au kutoa taarifa ya mambo muhimu yenye hasara za kiuchumi au za aina nyingine.

Kwa mujibu wa sheria iliyounda taasisi hiyo ya mwaka 1996 Idara ya Usalama wa Taifa inalojukumu la kukusanya na kuchambua habari mbalimbali ambazo zina umuhimu katika kuhakikisha kuna usalama, utulivu na utawala wa sheria nchini.

Kwa muda wa miaka kadhaa sasa hivi idara hiyo inaonekana aidha kulegalega, kuzembea au kutokuwa na uwezo wa kuwaza kukusanya habari nyeti na muhimu na kuzifanyia kazi inavyostahili. Hata hivyo tatizo kubwa la idara hilo linatokana na sheria yenyewe iliyoiunda ambayo inaikataza wazi kabisa idara hiyo kusimamia usalama nchini na hivyo kuiacha iwe ya kukusanya habari na kuvipatia vyombo vingine vyenye jukumu na nguvu za kisheria kukamata na kuwafikisha watu mahakamani.

Huko nyuma idara hiyo ilishindwa kufanya uchunguzi wa kina kwa kampuni ya Richmond ambayo iliingizwa nchini ili kuleta majenereta ya umeme. Kushindwa kwa kampuni hiyo kutimiza jukumu hilo kulidhihirika baada ya uchunguzi wa Kamati teule kuonesha kuwa kampuni hiyo siyo tu haina uwezo lakini haikuwa imesajiliwa nchini.

TISS ilishindwa kung'amua mapema kuwa ile rada ambayo serikali ya Tanzania ilikuwa imedhamiria kuinunua ilikuwa inauzwa kwa bei ya juu kuliko kawaida na ya kuwa katika mchakato wake watu mbalimbali walipewa mgao wa kuweza kufanikisha mradi huo uliogharibu karibu shilingi za Kitanzania Bilioni 50.

Ni kwa sababu hiyo mama mmoja ambaye ni mtumishi wa serikali aliyekuwa amekwama njiani kwa karibu masaa manne siku ya Jumatano alielezea tukio la wazee hao kufunga barabara kuwa ni "la aibu na linaonesha jinsi gani wanausalama wetu hawako karibu na wananchi".

Kufanikiwa kwa wazee hao kuweza kulitikisha jiji imekuwa ni alama nyingine ya jinsi gani vyombo vya usalama ikiwemo TISS na Polisi vimeshindwa kwa mara nyingine kupata habari muhimu kabla hawajachelewa.

Hivi karibuni katika ziara yake mkoani Mbeya Rais Kikwete alijikuta anasimamishwa na kundi la vijana eneo la Mwanjelwa ambao nao waliweza kujipanga vizuri na kuweza kuingilia kati msafara wa Rais na kumlazimisha Rais asimame hapo na kuzungumza nao kinyume na taratibu za kiprotokali.

Hata hivyo kilelel cha kushindwa kwa taasisi hii kimethibitika zaidi katika masuala yanayohusiana na wizi wa fedha za EPA na kuingiwa kwa mikataba mibovu ya madini iliyoligharimu taifa mabilioni ya dola.

Hata hivyo afisa mmoja wa Usalama wa Taifa aliyewasiliana na kijarida hiki kwa njia ya mtandao na kukataa kutajwa jina lake kwa sababu ya kisheria alisema kuwa "tatizo letu siyo hasa ndani humu bali ni muundo wa kisheria, ndio unatuzuia kufanya mambo mengi".

"Huko nyuma tulikua na uwezo wa kufanya mambo mengi japo kwa usiri sana lakini sasa hivi, tumebakia kuwa wasindikizaji tu." alisema afisa huyo ambaye amekuwa kwenye taasisi hiyo kwa karibu miaka 15.

Hivi karibuni Mbunge wa Kigoma Kaskazini Mhe. Zitto Kabwe alielezea uzito wa tatizo la Usalama wa Taifa alipotoa hotuba yake wakati wa kikao cha bajeti na kusema kuwa Bunge lazima liangalie sheria ili TISS iwe na ufanisi mkubwa.

Hata hivyo haijajulikana kama Bunge lina mpango wa kufanya hivyo karibuni.

Soma bure

EPA: ASILIMIA 52 TU ZARUDISHWA!

Na. Jessy L. Fundi



Yawezekana baadhi ya watu walimaliza kutazama au kusikiliza hotuba ya Rais ya mwisho wa mwezi Oktoba wakiwa na imani kuwa asilimia zaidi ya 76 ya fedha zilizoibwa kutoka Benki Kuu (akaunti ya EPA) na makampuni 22 zimerejeshwa.

Rais Kikwete akielezea kiasi kilichorudishwa alisema kuwa "Napenda kuwajulisha kuwa, taarifa nilizoletewa majira ya mchana leo, ni kuwa kiasi cha shilingi 69,326,437,650 kati ya shilingi 90,359,078,804 zilikuwa zimerejeshwa. Hii ni sawa na asilimia 76.7."

Sasa hakusema ni sawa na asilimia 76 ya fedha gani. Ni wazi alikuwa anamaanisha kuwa ni asilimia ya hizo Bilioni 90.3 na siyo bilioni 133 ambacho ndicho kiasi kinachodaiwa kuchotwa toka akaunti ya EPA.

Sasa tukichukulikia kuwa kiasi kilichorudishwa ni hizo Bilioni 69.3 kutoka 133 bilioni zilizochotwa tunaona kuwa kilichorejeshwa kweli ni asilimia 52 hivi ya fedha zote na siyo 76.

Kama waliochota fedha hizo walienda wakazitumia na kuzalisha mabilioni mengine ya faida je ina maana kuwa tulichorudishiwa ni "mtaji" tu na siyo hata fedha walizojipatia faida?
Kama mtu kakuibia ng'ombe jike, na huyo ng'ombe akazaa huko kwa mwizi na wewe ukampata mwizi wako na ukaona ana ndama ananyonyesha utakapomchukua huyo ng'ombe je huna haki na ndama wake?

Ninavyoona mimi (yawezekana nimekosea) kilichofanyika ni kuwa serikali ya Rais Kikwete imeenda kudai ng'ombe tu lakini kwa sababu inazojua imeamua kuwaachia ndama wezi wetu.

Kama walioiba fedha za EPA walizifanyia biashara ni haki kabisa kuwadai riba na adhau ya wizi wao. Kwenda kufurahia kurudishwa mtaji kama walikopa ni kutuzuga.

MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

KATUNI ZA WIKI


Picha za Wiki

JIUNGE NA TOVUTI YETU MPYA

http://www.mwanakijiji.com

(Kwa habari na hotuba ya ushindi ya Seneta Obama)

Jiandikishe kushiriki mijadala, kupata habari, kusikiliza muziki na matangazo ya moja kwa moja kila mwishoni mwa juma.







KUTOKA KWENYE MTANDAO

Hakuna namna ya mtu kuweza kupona au kuonewa, lazima nifanye Legal Analysis (uchambuzi wa kisheria) kwanza, cha msingi usiulize majalada mangapi, niulize afya yangu tu, niombe uzima tu, kila kitu utaona kitakavyokwenda — **DPP Eliezer Feleshi**

Kikwete ilikuwa juu yake kwa haraka sana awafichuwe mafisadi halafu awapeleke mahakamani na kwa haraka autatafutie dawa ubovu huo ili kwaharaka aoneshe ukweli na uaminifu wake lakini kashindwa kabisa kufanya hivo na badala yake amekuwa na kigeugeu kisichokwisha.– **Mwaikimba**

Ndugu Watanzania wenzangu; Kuhusu uchunguzi uliokuwa unaendelea kufanywa kuhusu yale makampuni 9, nasubiri taarifa yao mpya kuhusu maendeleo ya uchunguzi huo. Taarifa niliyopewa wiki mbili zilizopita zinaonyesha kuwa polisi wetu bado hawajapata majibu kutoka kwa wenzao katika nchi walizoomba msaada. Hivyo, nakusudia kuwataka waendelee kufuatilia kwa wenzao ili hatua zipasazo ziweze kuchukuliwa.— **Rais Kikwete**

Kwa kweli bongo viongozi hatuna. huyu ndio raisi jamani aliyeapa kutetea na kulinda katiba jamhuri ya muungano wa Tanzania. God have mercy on this country and its people.— **Anonymous**

Ripoti ya tume ya Philip Mangula aliyefanya uchunguzi kuhusu kukiukwa kwa maadili ya chama wakati wa CCM presidential primaries imepotelea wapi? nadhani wakati umefika ripoti hiyo ipatikane kwani inaweza sana kutusaidia kuelewa yanayoendelea sasa hivi Tanzania.—**Jokakuu**

Ushindi wa Obama si kwa watu Weusi na Waafrika tuu, bali ni kwa kila mtu ambaye siku zote amelelewa na kukuwa katika mazingira yanayomwambia kuwa yeye ni batili, nusu na hana thamani.Ushindi wa Obama ni sawa na kuvunja minyororo ya utumwa na ukoloni.—**Rev. Kishoka**

CHAPA NA MPATIE MTU MWINGINE BURE

Cheche za Fikra

Mchapishaji na Mhariri Mtendaji

M. M. Mwanakijiji

Timu ya Waandishi
Benjamin Mwalukasa— Mhariri

Freddy Katunzi—Habari za Siasa

Mahmoud Rashid—Habari mbalimbali

Jessica L. Fundi – Makala

Kwa kujiandikisha, maoni, habari, na ushauri

Tuandikie: **Mhariri@klhnews.com**

Tovuti: **http://www.mwanakijiji.com**

***Kanusho:** Mawazo yanayonukuliwa hayawakilishi msimamo au mawazo ya mchapishaji na utawala wa kijarida hiki.*